# OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

**SHULE YA SEKONDARI MASANGE JUU S.L.P 228 LUSHOTO**
**NAMBA YA SIMU 0754 323 775/0787 323 775**

# FOMU YA KUJIUNGA NA SHULE

**JINA LA MWANAFUNZI…………………………………….**

1.0 Ninafurahi kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2021. Shule ya sekondari **Masange Juu** ipo mkoa wa Tanga, wilaya ya Lushoto kata ya Gare na kijiji cha Masange.

2.0 Mhula wa masomo unaanza tarehe 11/01/2021 na unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 11/01/20201saa moja kamili asubuhi mwisho wa kuripoti ni tarehe 25/01/2021

## 3.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

### 3.1 Sare ya shule

a. Sare ya shule hii ni **kitambaa cha ugoro kwa suruali na sketi na shati nyeupe mikono mifupi** kwa wasichana na wavulana. Sketi itashonwa linda box moja mbele na moja nyuma

b. Kwa wale watakao shona hijabu watashona kitambaa sawa na wengine . watashona sketi ndefu na zisizo bana pamoja na juba linaloishia kwenye magoti la mikono mirefu

c. Sare ya michezo ni
   i. T-shirt ya timu ya taifa bluu au nyeupe
   ii. Viatu vya michezo

d. wanafunzi wote watashona tai ya kunyonga itakayofanana na kitambaa cha sketi na suruali .

e. viatu vya ngozi vyeusi vya kamba jozi mbili au zaidi

f. daftari kubwa kumi

NB: mwanfunzi atakae shone nguo fupi na suruali za kubana ( modo) hatapokelewa hivyo hakikisha unashona nguo zinazoendana na maadili ya kitanzania, suruali upana chini isipungue 16

### CHAKULA CHA MCHANA

Chakula cha mchana kinatolewa na wazazi kwa kuchangia nafaka hivyo mzazi unapaswa kuchangia nafaka kama taratibu zilivyowekwa na kamati ya chakula ya wazazi chini ya mtendaji wa kijiji. Fika shuleni utapewa utaratibu wa kukutana na mwenyekiti wa kamati ili aweze kukupa utaratibu. Mwanafunzi anaeshinda na njaa hafundishiki hivyo mzazi/ mlezi hakikisha mwanao anapata chakula cha mchana kwa afya na mustakabali wake kitaaluma.

## 5.0 KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE

i. Mwanafunzi wa shule ya sekondari Masange juu haruhusiwi kufika sehemu za baa na nyumba za kulala wageni bila sababu za msingi.
ii. Hairuhusiwi kufika kwenye nyumba za walimu bila ruhusa.
iii. Nimarufuku kwa mwanafunzi kutumia lugha ya matusi kwa mtu yeyote
iv. Hairuhisiwi kwa mwanafunzi kutumia madawa yakulevya kama vile mirungi, bangi pombe sigara na aina zozote zile za vilevi.
v. Mwanafunzi anapaswa kumsalimu yeyote Yule kwa nidhamu aliyemzidi umri.
vi. Kila mwanafunzi anapaswa kutumia lugha ya kiingereza masaa yote awepo shuleni na nje ya shule inapohitajika kufanya hivyo.
vii. Hairuhusiwi mwanafunzi kuwa na mahusiano ya / uasherati
viii. Hairuhusiwi mwanafunzi kufanya mgomo aidha kwa mwalimu au viongozi wengine wa ndani na nje ya shule.
ix. Kila mwanafunzi anapaswa kutii wimbo wa shule wimbo wa uzalendo na bendera ya Taifa popote pale awepo ndani na nje ya shule.

5.1. makosa yanaweza kusababisha mwanafunzi kufukuzwa shule.

i. Wizi
ii. Uasherati na ushoga
iii. Ubakaji
iv. Ulevi na matumizi ya dawa za kulevya
v. Kupigana au kupiga
vi. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma, ama mwenzako
vii. Kudharau bendera ya Taifa
viii. Kuoa au kuolewa
ix. Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule
x. Kutoa mimba
xi. Kugoma,kuchochea na kuongoza, au kuvuraga amani na usalama wa shule au watu.
xii. Kukataa adhabu kwa makusudi
xiii. Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi.

## 6.0. MAMBO MENGINE MUHIMU

a. Medical Examinition form ambayo itajazwa na mganga mkuu wa Hospitali ya serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporiti shuleni.
b. Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/mkataba wa kutoshiriki katika migomo,fujo na makosa yajinai
c. Fomuya mzazi kukiri kukubaliana na sheria ,kanuni, na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule

## 6.2. MWISHO

Nipende kuchukua fursa hii tena kukupongeza kwa kuchaguliwa kujiunga na shule ya sekondari masange juu, sambamba na hivyo tunawakaribisha sana shuleni kwetu.

**NB: kama mtoto wako anatatizo kubwa la kiafya ripoti kwa uongozi wa shule tatizo la mwanao ili lifahamike na tahadhali zichukuliwe. Liwe ni tatizo ambalo limethibitishwa na daktari**

. Nawatakia utekelezaji mwema

**…………………**

**KUPAZA A.J**

## OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

**SHULE YA SEKONDARI MASANGE JUU**
**S.L.P 228 LUSHTO**

…………………………………

…………………………………

…………………………………

…………………………………

## KUMB: KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MASANGE JUU

Mimi……………………………………….mzazi/mlezi wa…………………......

Nimesoma barua hii na kuyaelewa masharti ya shule. Nimeyakubali masharti hayo na sheria zote za shule. Nakiri kushirikiana na walimu pamoja na uongozi wa shule kuona kwamba mtoto wangu anafuata sheria hizi kikamilifu.

Jina la mzazi/mlezi………………………….……….. sahihi……………….tarehe………………

Mimi ……………………………………nimesoma kwa makini sheria zote za shule na kuzielewa, ninakubali sheria hizo na nitazifuata kikamilifu. Ninafahamu kwamba kitendo chochote kilicho kinyume na taratibu za shule kinastahili adhabu kali ikiwa ni pamoja na kufukuzwa shule.

Jina la mwanafunzi…………………………………..….sahihi……………. tarehe…………….

NB: fomu hii ijazwe na mzazi/mlezi na kurudishwa shuleni siku ambayo mwanafunzi anakuja kuripoti.

**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

SHULE YA SEKONDARI MASANGE JUU
S.L.P 228
**LUSHOTO**
**………………….**

The medical officer
……………………..................
………………………………

**REF: STUDENT'S MEDICAL EXAMINATION FORM**

(To be completed by a medical officer in respect of the student mentioned below)

a. Full student's name……………………………………………………..
b. Date of birth…………………………………………………………….
c. Blood Count ……………………………………………………………
d. Stool examination……………………………………………………….
e. Urinalysis………………………………………………………………….
f. Venereal Diseases Test…………………………………………………..
g. T.B. Test………………………………………………………………….
h. Eye Test………………………………………………………………….
i. Ear Test…………………………………………………………………..
j. Chest……………………………………………………………………..
k. Spleen…………………………………………………………………….
l. Abdomen………………………………………………………………..
m. Plan Test………………………………………………………………….

Additional Information (if any) for example Physical defects or impairment(s) for instance body parts, infections, family diseases or known affliction etc
…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………
………………………………………….

I certify that the above mentioned student is fit/unfit to pursue secondary Education studies
Name of officer……………………………………… signature………….
Date……………….
Official stamp